

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



26 Yoshua kiongozi mpya

Kwa Biblia Kumbukumbu la Torati mlango wa 34;
Yoshua mlango wa 1

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Musa alikuwa kiongozi shupavu aliyependa na kutii Mungu. Mungu alimchagua Yoshua kuwa kiongozi mpya. Mungu alimwambia awe na ujasiri na amwamini.

Somo

Waisraeli walikuwa wamesafiri jangwani kwa miaka arobaini. Mwishowe walifika kwa mpaka wa nchi ya Kanaani tena. Musa alikuwa amemaliza kazi yake. Alikuwa ameongoza Waisraeli kupita jangwani mpaka nchi ya ahadi. Mungu alikuwa amemwambia kwamba hataingia nchini kwa sababu alikaidi Mungu na kupiga mwamba mara mbili. Musa alikuwa na miaka 120 lakini alikuwa bado ana nguvu na afya.

Musa alikuwa mmoja wa manabii wa Mungu wa maana. Aliandika vitabu vyta kwanza vitano vyta Biblia. Musa alizungumza na Mungu mara nydingi. Aliona utukufu wa Mungu. Alikuwa shujaa na mzuri. Alikuwa na ujasiri mkuu tena kiongozi wa ajabu.

Mungu aliambia Musa aende juu ya mlima wa Nebo na atakufia huko. Kwanza Musa alibariki kabila zote za Waisraeli. Aliaga watu wake. Watu walijua kwamba Musa alikuwa kiongozi mzuri. Walilia wakati alikuwa akiwaaga. Hata watoto walilia walipojua Musa anaenda kukufia juu mlimani.

Maswali

1. Musa alikuwa na miaka mingapi?
2. Musa alikuwa kiongozi mzuri?
3. Mbona Waisraeli walilia?
4. Mungu aliambia Musa aende wapi?
5. Musa aliona nini alipokuwa juu ya Mlima wa Nebo?
6. Mbona Musa hakukubaliwa kuingia kwa nchi.
7. Musa ataenda kwa nchi lini?
8. Mungu alichagua nani kuwa kiongozi mpya?
9. Kazi ngumu ya Yoshua ilikuwa gani?
10. Mungu aliahidi Yoshua nini?

Majibu

1. Musa alikuwa na miaka 120.
2. Ndiyo, Musa alikuwa kiongozi mzuri.
3. Waisraeli walilia kwa sababu Musa alikuwa anaenda kufa.
4. Mungu alimwambia Musa aende juu ya mlima.
5. Musa aliona nchi yote ya Kanaani - nchi ya ahadi.
6. Kwa sababu alikaidi Mungu na kupiga mwamba mara mbili.
7. Musa ataenda kwa nchi wakati Yesu atarudi.
8. Mungu alichagua Yoshua kuwa kiongozi mpya.
9. Kazi ngumu ya Yoshua ilikuwa, aongoze Waisraeli washinde na kuchukuwa nchi.
10. Mungu aliahidi kwamba atamsaidia Yoshua kuwa kiongozi mzuri.

Musa alianza safari ndefu ya kuenda juu ya mlima wa Nebo. Watu walimfuata kwa mwendo mfupi. Mwishowe wakaambia Musa kwaheri. Musa alienda juu kwa kilele cha mlima.

Kabla Musa afe, Mungu alimwonyesha nchi ya Kanaani. Mlima wa Nebo ni mlima mrefu sana. Huko juu mlimani Musa aliona nchi yote. Aliona bonde la Yordani. Aliona n'gambo ya Bahari ya Kati. Aliangalia juu kaskazini na kuona Mlima wa Kameli na Lebanoni. Musa alifurahia kuona nchi ingawaje hakukubaliwa kuingia huko. Kwa hivyo Musa akakufia mlima wa Nebo na Mungu akamzika. Wingu ilifunika juu ya mlima. Waisraeli waliomboleza kifo cha Musa kwa siku thelathini.

Musa alikufa. Amekuwa kaburini asijue lolote huko mlimani. Yesu atakaporudi, atamfufua kutoka kwa wafu. Yesu atasimamisha Ufalme wa Mungu duniani. Hapo Musa atakuwa kwa huo Ufalme wa Mungu milele.

Mungu alichagua Yoshua kuwa kiongozi mpya. Yoshua alikuwa kiongozi mzuri lakini hakukuwa shupavu kama Musa. Yoshua alikuwa na kazi ngumu sana ya kufanya. Waisraeli walikuwa tayari kuingia kwa nchi ya ahadi. Lakini kwanza lazima washinde watu waliokuwa wakiishi kule. Wale watu walikuwa wa nguvu na wengine walikuwa majitu. Waliishi kwa miji ya kuta zilizokuwa za nguvu. Yoshua alitakiwa aamini Mungu. Alikuwa aongoze Waisraeli washinde ili wachugue nchi. Ilikuwa kazi ngumu ya kufanya.

Mungu ana nena na Yoshua. Mungu alisema atawaongoza na awasaidie kushinda na kuchukua nchi. Mungu aliahidi kusaidia Yoshua vile alisaidia Musa. Mungu alimwambia Yoshua awe jasiri na ajipe moyo. Mungu alimwambia kwamba akimwamini, atamsaidia

Yoshua alikuwa kiongozi mzuri kwa sababu aliamini na kupenda Mungu wakati wote. Walipotoka Misri, Yoshua alikuwa bado kijana mdogo. Alisafiri jangwani kwa miaka arobaini. Alijifunza kuwa shupavu na nguvu tena aliamini Mungu. Yoshua alikuwa mmoja wa wapelelezi walioletea Waisraeli habari njema.

Alikuwa na imani kwamba Mungu atawasaidia washinde kuchukua nchi. Kwa somo lifuatalo tutajifunza vile Yoshua alikuwa kiongozi mzuri na akaongoza Waisraeli mpaka nchini.

Safari ya Jangwani

